

Pareto

### **Mabadiliko ya ubora yaliyofanyiwa kikausho awali:**

- Haina haja ya kupiga msasa
- Kiwango cha mbao hupunguzwa
- Mashiko kwenye trei kuondolewa
- Gharama ya kutengeneza kupunguzwa
- Asilia zinazotumika kuwa za kawaida
- Utaratibu wa kufuata katika kubuni.



### **Kenya Agricultural Research Institute**

S.L.P.5781 I-00200, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Nukulishi: 254-20-4183344

Baruapepe: [resource.centre@kari.org](mailto:resource.centre@kari.org)

Tovuti: [www.kari.org](http://www.kari.org)

### **Watayarishaji:**

Wanjala, N., Busienei T. na P, Pertet, E.P.

### **Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:**

### **Mkurugenzi wa Kituo,**

KARI-Molo

S.L.P. 100, Molo

Simu: (051)721030, Nukulishi: (051)721030

Baruapepe: [nprckarimolo@yahoo.co.uk](mailto:nprckarimolo@yahoo.co.uk)

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 74 /2008

**Shilingi 20 za Kenya**

# **Tumia jamvi la miale ya jua kukausha pareto**



## Utangulizi

Wakulima wengi wanakausha pareto kwa kutumia jua moja kwa moja lakini vikaushio vya miale ya jua vinaweza kutumiwa pia.


Kikaushio cha miale ya jua kinaweza kutengenezwa kwa kutumia mbao zisizopigwa randa ili kuokoa wakati na kupunguza kazi.

## Jinsi ya kubuni kikaushio cha jua Mahitaji

Mbao	(c.s.a)	Urefu	Kiasi
Fremu	2½"X1"	68½"	3
	2"X1"	36"	3
Vifungio	½"X1"	70"	2
	½"X1"	37½"	2
Mhimili wa nyuma	4"X2"	42"	2
Mhimili wa mbele	4"X2"	45½"	2
Boroti ya kando	1½"X2"	68"	4
Boroti ya kando	1½"X2"	32"	4
Karatasi ya nailoni		53X94"	1

## Hatua ya kwanza: Fremu ya msingi

Kwa kutumia seti ya mraba na ukanda wa kupimia, laza mbao za urefu wa inchi 42, 45.5 na 32 kutoka kwa fremu na upigilie misumari zikiwa zimenyooka. Rudia hayo tena, na utengeneze fremu nyingine ili zive mbili. Ziunganishe hizo mbili ili kuunga moja kama inavyoonyeshwa hapa chini.



Fremu	(c.s.a)	Urefu	Kiasi
	4"X1"	35"	2
	4"X1"	61½"	2
	2"X1"	61½"	1
	2"X1"	35"	1
	2"X1"	26½"	4
	2"X1"	14½"	4
Viunganishi	½"X1"	60"	2
	½"X1"	30½"	2
Kizuizi cha rafu	2½"X1"	12"	1
Jamvi la kavirondo		59"X30"	1
Misumari		2½"	18pcs
		2"	16pcs
		3"	63pcs
		4"	30pcs

## Kupaka rangi


Rangi ya kwanza ya maji	lita 2
Rangi nyeupe ya mafuta	lita 2
Mafuta ya rangi	lita 1/2

## Ala zinazohitajika:

Nyundo, filifili ya umbo la ukanda wa chuma, pamoja na penseli ya kukoleza.

## Hatua ya pili: trei (chano)

Tumia vipande viwili vya mbao vyenye urefu wa inchi 59 na 34.5 na uviunganishe kama inavyoonyeshwa katika mchoro hapa chini. Jamvi linakatwa kulingana na ukubwa wa trei na kuwekwa chini ya trei kisha kishikilio kinatumiwa ili kuliweka jamvi mahali panapotakiwa.



## Hatua ya tatu: Paa

Fuata hatua zilizotumiwa katika ujenzi wa trei katika kujenga paa. Unganisha vipande vyote vya mbao na kuviwekelea juu ya fremu ya juu. Paa hilo lipigiliwe misumari pembe zote zinazoshikana.

## Hatua ya nne: Kupaka rangi

Rangi hupakwa baada ya uundaji wote kukamilika. Rangi nyeupe ya maji inatiwa kwanza kisha kuachwa ikauke siku moja na kufuatiwa masaa na rangi ya pili. Baada ya masaa manne, rangi ya mafuta inapakwa kisha kukaushwa kwa siku moja.



Kupaka fremu rangi

## Hatua ya tano: Karatasi ya nailoni

Karatasi ya nailoni yenye urefu wa inchi 53 kwa 94 inayoning'inia kwa urefu wa inchi 16 katika kila upande hukatwa na kuwekelewa kwenye viunganshi vilivyobuniwa wakati wa kutengeneza paa. Zinapigiliwa misumari na kikausho kiko tayari kwa matumizi.